

KANISA KATOLIKI JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM
PAROKIA YA MT. YAKOBO MKUU MTUME – KIJITONYAMA

S.L.P 34057, Dar es Salaam –Tanzania.Email :-kijitonyamaparish2016@gmail.com

HISTORIA YA PAROKIA

Historia yetu ilianza Mnamo **Mwaka 1992** kama kituo cha Sala katika Shule ya Msingi Kijitonyama, Waumini wenzetu wakiongozwa na Mzee Selius Mpasha na Bi.Hilda Swai,wakati huo baadhi yao walikuwa wakisali Parokia ya Mwenge na wengine Parokia Mama ya Mwananyamala.

Waasisi hao walikubaliana kupeleka maombi ya kuanzishwa **Kituo cha Sala** hapa Kijitonyama. Baada ya kufanyiwa kazi maombi hayo na Baba Paroko wa Parokia ya Mwananyamala Padri Thadeus Mshanga,tulipata ruhusa ya kusali Kituoni hapo. Tuliendelea kusali pale hadi Serikali ilipoagiza kuwa taasisi zote za Dini zisitumie tena majengo ya shule kwa ajili ya Ibada.

Ndipo mwishoni mwa **Mwaka 1999**, tulipata eneo Mahali tulipo sasa na tukajenga **Nyumba ya Sala**. Mnamo **Mwaka 2000** katika mkesha wa Krismasi tulihamia rasmi. Tuliendelea kusali kama kituo cha Sala hadi **Mwaka 2002** tulipopandishwa hadhi na kuwa **Kigango cha Kijitonyama** chini ya Parokia ya Mwananyamala iliyokuwa ikiongozwa na Baba Paroko Padri Priscus Jumamosi.

Baada ya kuwa Kigango tuliendelea kusali na kuongeza maeneo ya Kanisa na kuimarisha mahitaji ya Kiroho kwa waumini.Mwishoni mwa **Mwaka 2015** baada ya uzinduzi wa nyumba ya Mapadri, Kigango cha Kijitonyama kilipatiwa Padri Kiongozi ambae alikuwa msimamizi wa shughuli zote za Kichungaji hapa Kijitonyama.

Tarehe 06/01/2016 Siku ya Epifania, Kigango cha Kijitonyama kilitangazwa rasmi kuwa **Parokia Teule ya 90 katika Jimbo kuu la Dar eS Salaam**.

Tarehe 26/04/2016 ndiyo siku ambayo ndoto na Maombi ya Waamini wa Kijitonyama yalipotimia kwa kujibiwa na Mwenyezi Mungu pale Parokia Teule ya Kijitonyama ilipopandishwa hadhi na kuwa **Parokia Kamili ya Mt. Yakobo Mkuu Mtume Kijitonyama** chini ya **Baba Paroko wa kwanza Padri Arnold Babu Tarimo.**

MAPADRI NA WENYEVITI WALIOONGOZA KWA NYAKATI TOFAUTI

1. Mwaka 1998-2001-Kamati Tendaji iliyoongozwa na Mzee Senyon ambae sasa ni Marehemu chini ya Baba Paroko Padri Benedict Ndeyikio.
2. Mwaka 2001-2004-Kamati Tendaji iliongozwa na Mzee Mapunda chini ya Baba Paroko Padri Moria ambae kwa sasa ni Marehemu.
3. Mwaka 2004-2007-Kamati Tendaji iliongozwa na Mzee Crispini Libana ambae kwa sasa ni Marehemu chini ya Baba Paroko Padri Moria ambae kwa sasa ni marehemu.
4. Mwaka 2007-2010-Kamati Tendaji iliongozwa na Gabinusi Maganga chini ya Baba Paroko Padri Focus Massawe.
5. Mwaka 2010-2012-Kamati Tendaji iliongozwa na Novatus Panda chini ya Baba Paroko Padri Focus Masawe.
6. Mwaka 2012-2016-Kamati Tendaji iliongozwa na Gabriel Kimaro chini ya Baba Paroko Padri Focusi Masawe tukiwa Kigango mpaka tulipokuwa Parokia Kamili tukiwa chini ya Paroko Mpya Padri Arnoldi Babu Tarimo